
# Bima dhidi ya madhara yanayotokana na uhalifu wa ndovu nchini Kenya na Sri Lanka

Mradi huu utawezesha masoko binafsi kuwapa bima wakulima wadogo nchini Kenya na Sri Lanka kutokana na uharibifu unaosababishwa na migogoro kati ya wanyamapori na binadamu hasa kutoka kwa ndovu



iied

IPS

ab consultants
your microinsurance partner

# Kwa kifupi

Mradi huu utawezesha masoko binafsi kuwapa bima wakulima wadogo nchini Kenya na Sri Lanka kutokana na uharibifu unaosababishwa na migogoro kati ya wanyamapori na wakaazi hasa kutoka kwa tembo. Pia itaunga mkono bima katika nchi mbili - Kenya na Sri Lanka - ambapo migogoro kati ya wanyamapori na wakaazi ni tishio kubwa kwa maisha na mazingira. Wauzaji wa bima binafsi kutoka nchi hizi mbili pia wana tamanio na lengo la kujaza pengo la ukosaji wa bima kwenye soko ya nchi zote mbili.

## Kwa nini sasa?

Migogoro ya Wanyamapori (HWC) husababisha gharama kubwa za kiuchumi na za kibinadamu kwa watu wa mapato  ya chini katika sehemu nyingi za dunia, hasa karibu na maeneo yaliyohifadhiwa. Ndovu ni chanzo kikubwa cha migogoro kati ya wanyamapori na wakaazi katika Afrika na Asia. Wanaharibu na kula mazao, kuharibu mali, na wakati mwingine kuumiza na hata kuwaua binadamu. Kila mwaka, karibu watu 35 wanauawa na ndovu nchini Kenya na hadi 80 watu nchini Sri Lanka.

Mara nyingi hii inasababisha wakaazi kuwaua wanyamapori  moja kwa moja ili kujikinga au kulipiza kisasi kwa kuwasaidia wawindaji haramu. Kila mwaka, maafisa wa kulinda pori huwapiga risasi ndovu waharibifu kati ya 50 na 120 nchini Kenya. Kuzidisha, zaidi ya ndovu 230 huuwawa na wakulima nchini Sri Lanka. Nchini Sri Lanka, ndovu wameorodheshwa kati ya wanyapori waliohatarishwa, waliobaki porini  wakikadiriwa kuwa kati ya 2,500-4,000. Kiwango hiki kinawakilisha  50% katika kipindi cha miaka 60-75.

Ulimwenguni, hatua nyingi tofauti zimejaribu kupunguza migogoro kati ya wanyamapori na wakaazi. Hatua hizi zimekuwa ni za kifedha pamoja na uhifadhi lakini hazijafanikiwa. Bima ya kibinafsi imetumika kama mkakati mbadala kwa idadi ndogo, lakini hadi sasa kuna juhudi chache za kuyahusisha makampuni ya bima ya kibiashara. Hata hivyo nchi za Kenya na Sri Lanka, zilianza kuchunguza uwezekano wa mipango ya aina hiyo. Mradi huu una nia ya kusaidia serikali za nchi hizo mbili kuendesha majaribio mapya ya mipango ya bima, kujifunza kutoka kwa kila mmoja, na kuendeleza mbinu ya kitaifa yenye ufanisi. Utafiti huu utazingatia changamoto nne muhimu:

- Uthibitishaji wa gharama  kwa ufanisi
- Malipo ya wakati unaofaa na ya haki
- Kuepusha motisha ya migogoro na kuunganisha malipo na ustawi mzuri
- Ustawi wa kifedha kwa wakaolipia bima peke yao

Utafiti utatoa masomo kutoka kwa nchi hizi mbili zinazozingatiwa. Masomo haya yanaweza tumika kutaarifu uendelezaji wa miradi kama hiyo mahali pengine.

## Tamanio letu

Mradi huu unatarajiwa kupunguza migogoro kati ya binadamu na ndovu ambayo imesababishwa moja kwa moja na uongezeko wa shughuli za binadamu ndani ya makazi ya wanyamapori. Shughuli hizi ni kwa njia ya kuingilia makaazi ya ndovu na njia zake za uhamiaji. Inatarajiwa kwamba mradi utakapokamilika, hasara na uharibifu kutokana na migogoro ya ndovu na binadamu katika nchi zote mbili utapungua kwa angalau 20% kwa wakulima wote wa kike na kiume watakaopata bima. Inakadiriwa pia kuwa kufikia mwisho wa mradi, bima binafsi itakayoanzishwa itapunguza vifo vya tembo kutokana na migogoro ya binadamu kwa 10% nchini Kenya na 10% nchini Sri Lanka kama inavyooneshwa hesabu na taarifa za serikali.

# Matarajio kutoka na Matokeo ya mradi

## Matarajio kutoka IIED

1. Kutoa msaada wa kiufundi kusaidia mfumo wa kitaifa wa kutoa bima dhidi ya mgogoro wa wanyamapori na binadamu nchini Kenya kulingana na sheria ya 2013 ya uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori.
2. Kutoa msaada wa kiufundi kwa majaribio ya mipango ya bima dhidi ya ya mgogoro wa wanyamapori nchini Sri Lanka
3. Kujadili utendakazi bora wa kimataifa kwa majukumu ya mashirika ya bima binafsi inayoshughulikia mgogoro kati ya wanyamapori na binadamu

## Matokeo ya mradi

1. Kubuni bima ya kitaifa dhidi ya mgogoro kati ya wanyamapori na binadamu itakayowafaidi wakulima wa kike na kiume nchini Kenya kabla ya kukamilika kwa kipindi cha mradi, itakayo simamiwa na makampuni ya bima ya kibinafsi.
2. Bima ya kitaifa dhidi ya mgogoro kati ya wanyamapori na binadamu itakayowafaidi wakulima wa kike na kiume nchini Sri Lanka, katika maeneo yaliyochaguliwa na mradi na kusimamiwa na mashirika ya bima ya kibinafsi kabla ya kukamilika kwa mradi.
3. Makubaliano ya utendakazi bora bora wa kimataifa kwa majukumu ya mashirika ya bima binafsi ili kupunguza mgogoro kati ya wanyamapori na binadamu.



# Ratiba ya shughuli

## Mwaka 1

- Vikao vya mipango ya kuanzilisha mradi nchini Kenya na Sri Lanka
- Utafiti na uchambuzi wa taarifa zitakazoeleza idadi ya vifo vya binadamu na uharibifu unaosababishwa na ndovu nchini Kenya na Sri Lanka wakati wa kuanzilisha mradi
- Ubunifu wa mpango wa bima na AB Consultants nchini Kenya na IPS nchini Sri Lanka. Mipango ya Bima itakaguliwa na IIED.
- Kusoma fasihi na taarifa zilizopo kuhusu mipango ya malipo ya visa vya migogoro kati ya binadamu na wanyamapori na bima husika zilizopo

## Mwaka 2

- Ukamilishaji wa ubunifu wa bima nchini Kenya na Sri Lanka
- Mazungumzo ya kitaifa nchini Kenya na Sri Lanka
- Utekelezaji wa ima iliyobuniwa nchini Kenya na Sri Lanka
- Ufuatiliaji, ujiandikishaji, utekelezaji na ufanisi wa bima iliyobuniwa kupitia kwa utafiti wa familia, mahojiano na kampuni za bima nnchini Kenya na Sri Lanka.
- Kuandika masomo, matokeo na mapendekezo itakayotumiwa na washirika nchini Kenya na Sri Lanka

## Mwaka 3

- Mazungumzo ya kitaifa nchini Kenya na Sri Lanka
- Barua ya kuthibitisha kuhusika kwa serikali na kampuni za bima katika uanzilishaji wa mradi
- Kulinganisha masomo kutoka kwa nchi zote mbili kulingana na ripoti za kitaifa zitakazoandikwa
- Semina ya mwisho ya kitaifa
- Usambazaji wa taarifa na shuguli za kufikia wahusika na wadau





# Wahusika kwenye mradi

## International Institute for Environment and Development (IIED)

IIED ni Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo. IIED ititatoa uangalizi wa jumla wa kiufundi, kuratibu mradi, kusimamia mikataba ya wahusika na kutoa ripoti ya wafadhili kwa DEFRA. Katika usimamizi wa kiufundi IIED itaongoza mapitio ya mipango ya kimataifa ya bima iliyopo mwanzoni mwa mradi na mafunzo yatakayokuwa yamejitokeza kutoka miradi ya nchi zote mbili kufikia mwisho wa kipindi cha mradi; ikiunganisha taasisi za ngazi za kitaifa nchini Kenya na Sri Lanka na wataalam wa kimataifa na watekelezaji. IIED ni shirika la utafiti wa sera na hatua za utafiti. IIED inasisitiza na kuunga mkono maendeleo endelevu ili kuboresha maisha na kulinda mazingira ambayo wakaazi wanajengea maisha yao. Utaalam wa IIED ni katika kuunganisha vipaumbele vya wakaazi wa maeneo wanakofanya kazi na  changamoto za kimataifa. Makao makuu ya IIED yako jijini London kule uingereza na kazi zao hufanyika Barani Afrika, Bara Hindi, Marekani, Marekani ya Kusini, Mashariki ya Kati na maeneo ya bahari Pasifiki, wakihudumia baadhi ya watu walio na mazingira magumu zaidi duniani.

## AB consultants, Kenya

AB Consultants ni washauri wa bima kutoka Kenya. Washauri wa AB wataongoza shughuli ya muundo wa mpango wa bima nchini Kenya. Washauri wa AB ni shirika huru lenye lengo la kusababisha ongezeko la kupenya kwa bima nchini Kenya na sehemu nyinginezo Barani Afrika na hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa kusisitiza na kuzingatia bima zinzowafaa na kuwanufaisha watu wa matato ya chini na waliokosa kuhusishwa kwa mipango ya bima za kawaida.

## Institute of Policy Studies (IPS), Sri Lanka

IIPS ni Taasisi ya Mafunzo ya Sera nchini Sri Lanka. IPS itaongoza kazi ndani ya mazingira husika kwenye mradi nchini Sri Lanka. IPS ilianzishwa na Sheria ya Bunge mwaka wa 1988 na kufanywa rasmi taasisi ya kisheria mwezi wa Aprili, 1990.  IPS imejiimarisha kama taasisi inayoongoza kwa utafiti wa sera nchini Sri Lanka na imepata kutambulika katika eneo la Bara Hindi Kusini kwa uhuru wake na ubora katika utafiti wa sera. Usimamizi wa mazingira na rasilimali za kiasili pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa ni vipaumbele muhimu vya utafiti. IPS ilianzisha utafiti wa kuchunguza bima ya hali ya hewa kwa wakulima wa eneo kavu huko Sri Lanka wakifadhiliwa na fedha za msaada kutoka kwa ushirikiano wa mashirika ya maendeleo duniani linalofahamika kwa kizungu kama Global Development Network(GDN). Hii ilijumuisha idadi ya uchunguzi wa haja ya bima dhidi ya migogoro kati ya Wanyamapori na binadamu.

# Jihusishe

## Tembelea tovuti yetu

Maelezo ya mradi inapatikana kwenye mtandao na matokeo yatatolewa mradi utakavoendelea. https://www.iied.org/livelihoods-insurance-elephants-life-kenya-sri-lanka

## Wasiliana nasi

**IIED -** Paul Steele
paul.steele@iied.org

**IIED -** Dilys Roe
dilys.roe@iied.org

**IPS -** Athula Senaratne
athula@ips.lk

**AB Consultants -** Barbara Chabbaga
barbara.chabbaga@abconsultants.co.ke

Project Materials

**Economics; Biodiveristy**

*Keywords:*
Wildlife, Small-scale farming, Livelihoods

## Kuhusu wafadhili wetu

**Mpango wa Darwin ni mpango wa msaada kutoka kwa serikali ya Uingereza unaosaidia kulinda viumbe hai na mazingira ya kiasili kupitia kwa miradi ndani ya eneo husika. Mpango huu unafadhili miradi inayosaidia nchi zenye utajiri wa viumbe hai lakini zinashida ya umaskini wa rasmali ya kifedha unaowakwaza kufikia malengo yao chini ya makubaliano mbali mbali ya kimataifa kuhusu viumbe hai.**

Kwa ufadhili wa mpango wa Darwin

DARWIN INITIATIVE

## Photo credits:

Front cover: Photo by Larry Li on Unsplash

Page 2: Photo by Bread for the World from Flickr via creative commons/ Photo by Dhammika Heenpella from Flickr via creative commons

Page 4: Photo by Sutirta Budiman on Unsplash